TANGAZO LA SERIKALI NA.110 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

(*Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA SEEKE YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Seeke ya Mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango miji na Mkurugenzi wa Manispaa ya Kahama.

________

JEDWALI

________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira – nukta 448875.14MS, 9578135.07KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa KS$18^{O}$04’56.14”MS kwa umbali wa kilomita 3.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira – nukta 450039.58MS, 9574570.09KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi kwa kufuata hifadhi ya mlima Seeke katika uelekeo wa KS$76^{0}$56’05.20”MG kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira – nukta 448854.76MS, 9574295.84KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ$18^{0}$04’56.14’’MG kwa umbali wa kilomita 3.6 hadi kwenye alama ya mpaka upimaji namba D yenye majira – nukta 446927.07MS, 9577352.27KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi katika uelekeo wa KZ$68^{0}$06’08.29’’MG kwa umbali wa kilomita 2 hadi ulipoanzia.”

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*